# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1022

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-841-5

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA SAIKOLOJIA NA SOSHOLOJIA YA ELIMU
# STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA MSINGI
# 2023

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2023
Toleo la Kwanza, 2023

ISBN: 978-9987-09-841-5

Taasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P 35094
14112 Dar es Salaam.

Simu: +255 735 041 168 / 735 041 170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu Msingi.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha wala kutafsiri Muhtasari huu kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolaojia.

# Yaliyomo

Orodha ya Majedwali ........ v

Shukurani ........ vi

1.0 Utangulizi ........ 1

2.0 Malengo Makuu ya Elimu ........ 1

3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu ........ 2

3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu ........ 2

3.2 Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu ........ 2

4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu ........ 2

5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu kwa Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi ........ 3

6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4

6.1 Mkufunzi ........ 4

6.2 Mwalimu tarajali........................................................................................................ 4

6.3 Mzazi/mlezi ............................................................................................................. 5

7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ....................................................................... 5

8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji .......................................................................... 6

9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji ...................................................................... 6

10.0 Idadi ya vipindi ...................................................................................................... 7

11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji.................................................................. 7

Bibliografia ................................................................................................................... 11

# Orodha ya Majedwali

Jedwali Na. 1: Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo kwa Mwaka wa Kwanza na wa Pili .......... 3
Jedwali Na. 2: Alama za Upimaji Endelevu .......... 7
Jedwali Na. 3: Maudhui ya Mwaka wa Kwanza .......... 8
Jedwali Na. 4: Maudhui ya Mwaka wa Pili .......... 10

# Shukurani

Maandalizi ya muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha kupatikana kwa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala. Vilevile, Taasisi inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la maboresho ya Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu ni Somo la lazima katika Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi. Ujifunzaji wa somo hili utamwezesha mwalimu tarajali kuwa na uwezo wa kutumia misingi ya saikolojia na sosholojia ya elimu, kanuni na nadharia za ujifunzaji katika ufundishaji na ujifunzaji wa mwanafunzi. Aidha, somo hili litamwezesha mwalimu tarajali kutoa ushauri na unasihi kwa mwalimu tarajali ili kuwa na tabia na mienendo inayokubalika katika jamii. Vile vile somo hili litamwezesha mwalimu tarajali kuijua jamii yake na kujenga mahusiano chanya kati yake na mwanafunzi ili tendo la ufundishaji na ujifunzaji liweze kufikiwa kwa ufanisi.

Muhtasari huu umeandaliwa ili kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa Saikolojia na Sosholojia ya Elimu ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi Tanzania Bara. Muhtasari unatoa maelekezo ya kuwawezesha mkufunzi kuandaa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu tarajali kwa ufanisi. Vilevile, muhtasari unatoa nafasi kwa wakufunzi kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ulimu.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba ili kuweza kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya Taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na
(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo Kuu la Elimu ya Ualimu

Kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo mahususi ya Elimu ya Ualimu ni kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;
(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;
(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali kwa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji;
(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, *classroom-based action research*).

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu

Muhtasari wa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu unalenga kumwezesha mwalimu tarajali:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(a) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;
(b) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji wa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;
(c) Kutumia, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(d) Kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(e) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (*instructional leadership*); na
(g) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, *classroom-based action research*).

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi

Muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi una umahiri mkuu na umahiri mahususi kama inavyojitokeza katika jedwali Na.1.

**Jedwali Na. 1:** *Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi wa Somo kwa Mwaka wa Kwanza na wa Pili*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu saikolojia ya elimu katika ufundishaji na ujifunzaji | 1.1 Kumudu misingi ya saikolojia ya elimu |
| | 1.2 Kuchambua hatua za makuzi na maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji |
| | 1.3 Kumudu nadharia na kanuni za ujifunzaji |
| | 1.4 Kumudu stadi za ushauri na unasihi kwa mwanafunzi |
| 2.0 Kumudu sosholojia ya elimu katika ufundishaji na ujifunzaji | 2.1 Kumudu misingi ya sosholojia ya elimu |
| | 2.2 Kuchambua masuala ya kijamii yanayoathiri malezi na ujifunzaji wa mwanafunzi |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji katika somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi unategemea ushirikiano baina ya Mkufunzi, Mwalimu tarajali na Mzazi/Mlezi katika kutimiza wajibu wao ambao ni:

### 6.1 Mkufunzi

Mkufunzi anatarajiwa:

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki;

### 6.2 Mwalimu tarajali

Mwalimu tarajali anatarajiwa:

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri stahiki katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ufundishaji na ujifunzaji, mbinu za kufundishia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia na kujifunzia, kuandaa na kutumia vifaa vya kufundishia, kujifunzia na kutathmini mwanafunzi;

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

### 6.3 Mzazi/mlezi

Wajibu wa mzazi/mlezi anatarajiwa:

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika shughuli za ujifunzaji.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Muhtasari huu unasisitiza matumizi ya mbinu za ufundishaji na ujifunzaji zinazolenga kumwezesha mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi atatumia mbinu shirikishi kumwezesha mwalimu tarajali kujifunza kwa kuzingatia mahitaji anuai na uwezo wake. Mbinu hizo ni pamoja na zile zinazomwezesha mwalimu tarajali kufikiri, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali na kushiriki katika kutoa mrejesho. Njia nyingine ni ziara za kimasomo, majadiliano katika vikundi, kazi za vitendo, kazimradi, utafiti, majaribio ya kisayansi na nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji.

Masuala mtambuka yatafundishwa kwa kuyachopeka wakati wa vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji katika masomo bebezi. Vilevile, ufundishaji na ujifunzaji unategemea ushirikiano baina ya mwalimu, mwanafunzi na mzazi/mlezi.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinazokidhi mahitaji ya ujifunzaji. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha mwalimu tarajali anapata nafasi ya kuona, kusikia, na kugusa/kuhisi bila kuathiri afya yake. Aidha, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa zimsaidie mwalimu tarajali kuelewa kinachofundishwa. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yanayomzungumka. Zana za ufundishaji na ujifunzaji zilizopendekezwa ni pamoja na matini zenye vifungu vya habari zinazohusu saikolojia na sosholojia ya elimu, manila zenye taarifa za saikolojia na sosholojia ya elimu, chatipindu zenye maandiko ya saikolojia na sosholojia ya elimu, matini za kibunifu na zisizo za kibunifu kuhusu saikolojia na sosholojia ya elimu, michoro ya kisaikolojia, picha, vitu halisi, kamusi za kisaikolojia na kisosholojia, na kadi za alama za uakifishaji. Zana zimependekezwa katika jedwali la maudhui katika safu ya zana.

## 9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji ni suala muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Upimaji wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya elimu utafanyika sambamba na masomo mengine yanayofundishwa katika ngazi ya Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi. Upimaji huu utamwezesha mkufunzi kupima umahiri wa mwalimu tarajali katika kumudu somo la Saikolojia na Sosholojia ya elimu. Aidha, utamwezesha mkufunzi kufuatilia kwa karibu maendeleo ya ujifunzaji ya mwalimu tarajali. Upimaji wa maendeleo utazingatia vigezo vilivyoainishwa katika kila shughuli ya ujifunzaji. Kwa hiyo, zana/vifaa vinavyotumika katika upimaji ni pamoja na mazoezi, maswali ya ana kwa ana, majaribio, hojaji, mkoba wa kazi, kazimradi, na mitihani ya muhula.

Katika kuamua kiwango cha ufaulu wa mwalimu tarajali upimaji wa mwisho (tamati) utachangia asilimia sabini (70%) na upimaji endelevu utachangia asilimia thelathini (30%). Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia hamsini (50%) na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafikisha asili mia hamsini (50%), mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

**Jedwali Na. 2:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| Na | Shughuli za upimaji | Mgawanyo (%) |
|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 2 | Mtihani wa Mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 3 | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Pili | 6.0 |
| 4 | Kazi mradi | 7.0 |
| 5 | Mkoba wa Kazi | 5.0 |
| | **Jumla** | **30** |

## 10.0 Idadi ya vipindi

Muhtasari wa Somo la Saikolojia na Sosholojia ya Elimu Stashahada ya Ualimu Elimu ya Msingi, unakadiria muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwalimu tarajali. Makadirio ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi viwili (2)

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya muhtasari huu yamegawanyika katika sehemu kuu sita ambazo ni: umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana/vifaa na idadi ya vipindi kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 3 na 4.

**Jedwali Na. 3:** *Maudhui ya Mwaka wa Kwanza*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu saikolojia ya elimu katika ufundishaji na ujifunzaji | 1.1 Kumudu misingi ya saikolojia ya elimu | (a) Kuchambua dhana na misingi ya saikolojia ya elimu *(maana chimbuko, mawanda, umuhimu na malengo)* | Dhana na misingi ya saikolojia ya elimu imechambuliwa kwa kuzingatia maana chimbuko, mawanda, umuhimu na malengo. | Vitabu vya Saikolojia,Vielelezo Wasifu wa wanasaikolojia, Chati ya chimbuko la saikolojia | 17 |
| | 1.2 Kuchambua hatua za makuzi na maendeleo ya mwanafunzi katika ujifunzaji | (a) Kuchambua hatua na nyanja za makuzi na maendeleo ya mwanafunzi na mahitaji yake ya msingi katika ujifunzaji *(nadharia, nyanja, hatua, mahitaji)* | Hatua na nyanja za makuzi na maendeleo ya mwanafunzi na mahitaji yake ya msingi katika ujifunzaji zimechambuliwa kwa kuzingatia nadharia, nyanja, hatua na mahitaji. | Vitabu vya Saikolojia, Chati za hatua za makuzi, Video fupifupi za ushauri nasaha, Makala/majarida, Visa mafunzo | 17 |

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.3 Kumudu nadharia na kanuni za ujifunzaji | (a) Kuchambua nadharia na misingi ya ujifunzaji *(maana, nyanja, kanuni, umuhimu, matumizi)* | Nadharia na misingi ya ujifunzaji imechambuliwa kwa kuzingatia maana, nyanja, kanuni, umuhimu, na matumizi katika ufundishaji | Vitabu vya Saikolojia, Ramani ya dhana *(concept map)* Video fupifupi za ushauri nasaha, Mihtasari na masomo husika | 17 |
| | 1.4 Kumudu stadi za ushauri na unasihi kwa mwanafunzi | *(a) Kuchambua nadharia, misingi na kanuni za ushauri na unasihi (maana, nadharia, aina za unasihi,umuhimu, tofauti, stadi, kanuni)* | Nadharia, misingi na kanuni za ushauri na unasihi zimechambuliwa kwa kuzingatia maana, nadharia, aina za unasihi, umuhimu, tofauti, stadi na kanuni. | Visa mafunzo, Matini ya saikolojia | 17 |
| | | (b) Kuchambua maadili na miiko ya unasihi (umuhimu, sifa za mnasihi,maadili, miiko) | Maadili na miiko ya unasihi zimechambuliwa kwa kuzingatia umuhimu, sifa za mnasihi,maadili na miiko. | Vitabu vya ushauri na unasihi, Visa mafunzo, Ramani ya dhana, Video fupifupi za ushauri nasaha | |

**Jedwali Na. 4:** *Maudhui ya Mwaka wa Pili*

| Umahiri Mkuu | Umahiri Mahususi | Shughuli za Ujifunzaji | Vigezo vya Upimaji | Zana zinazopendekezwa | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2.0 Kumudu sosholojia ya elimu katika ufundishaji na ujifunzaji | 2.1 Kumudu misingi ya sosholojia ya elimu | (a) Kuchambua nadharia na misingi ya sosholojia ya elimu (maana, chimbuko, nadharia, umuhimu na malengo) | Nadharia na misingi ya sosholojia ya elimu imechambuliwa kwa kuzingatia maana, chimbuko, nadharia, umuhimu na malengo. | Vitabu vya Sosholojia ya elimu, Wasifu wa wanasosholojia, Chati ya chimbuko la sosholojia, Ramani ya dhana, Video fupifupi za ushauri nasaha | 35 |
| | 2.2 Kuchambua masuala ya kijamii yanayoathiri malezi na ujifunzaji | (a) Kuchambua uhusiano wa shule na jamii katika malezi na ujifunzaji (wadau sosholojia ya elimu, umuhimu wa kujifunza uhusiano wa shule na jamii na michango na umuhimu wao katika uboreshaji wa malezi na ujifunzaji) | Uhusiano wa shule na jamii katika malezi na ujifunzaji umechambuliwa kwa kuzingatia wadau, michango yao katika uboreshaji wa malezi na ujifunzaji na umuhimu wake. | Vitabu vya sosholojia ya elimu, Chati ya mwingiliano wa mahusiano kati ya wadau wa sosholojia, Makala/majarida, Ramani ya dhana ya mwingiliano wa wadau wa sosholojia ya elimu | 35 |

# Bibliografia


Alexander, P. A., & Winne, P. H. (2012). *Handbook of educational psychology*. Routledge.

Bond, T. (2015). Standards and ethics for counselling in action, 1-352

Boronski, T., & Hassan, N. (2020). *Sociology of education.* Sage publication.

Capuzzi, D., & Stauffer, M. D. (2016). *Counselling and psychotherapy: Theories and interventions*. John Wiley & Sons.

Davies, S., & Guppy, N. (2010). *The schooled society: An introduction to the sociology of education*. Oxford University Press.

Duchesne, S., & McMaugh, A. (2018). *Educational psychology for learning and teaching*. Cengage AU.

Katitia, D. M. O. (2015). Teacher Education Preparation Program for the 21st Century. Which Way Forward for Kenya? *Journal of Education and Practice*, 6 (24), 57-63.

Kimokoti, A. C., & Kibera, L. W. (2007). *Fundamentals of sociology of education: With reference to Africa*.

Langford, P. E. (2004). Vygotsky's developmental and educational psychology.

MoEC. (1997). *Syllabus for Diploma in Education*. MoEC.

MoEST. (2019). *National Curriculum Framework for Basic and Teacher Education*. TIE:

Nevid, J. S. (2012). *Psychology: Concepts and applications*. Cengage Learning.

Nevid, J. S. (2021). *Essentials of psychology: Concepts and applications*. Cengage Learning:

Nezhad, A. S., & Vahedi, M. (2011). The Role of Educational Psychology in Teacher Education Programs. *Social and Behavioural Sciences* (30), 327 – 330

Okihara, Y. (1986). The Wide-Ranging Nature of the Japanese Curriculum and Its Implications for Teacher-Training. *Comparative Education*, 22(1), 13–18.

*Prout, H. T. (2007).* Counselling and psychotherapy with children and adolescents*: Historical,* developmental, integrative and effectiveness perspectives. *Counselling and psychotherapy with children and adolescents: Theory and practice for school and clinical settings*, 1-31.

Salkind, N. J. (Ed.). (2008). *Encyclopedia of educational psychology*. SAGE publications.

Slavin, R. E. (2014). *Educational psychology*: *Theory and practice*. Pearson Higher Ed. Teacher training in Norway retrieved from https://www.european-agency.org/sites/default/files/Teacher-Training-in-Norway.pdf

Slavin, R. E., & Davis, N. (2006). *Educational psychology: Theory and practice*.

TIE (2003). *Moduli ya Somo la Misingi ya Elimu: Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti.*TIE

TIE. (2013). *Mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti elimu ya msingi*: *Moduli ya kujifunzia somo la ualimu.* TIE.

WyEST. (2020). *Mwongozo wa malezi na unasihi na ulinzi wa mtoto kwas hule na vyuo vya ualimu Tanzania. Dodoma*: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

MoEST. (2022). *Safe schools programe for secondary schools*. Dodoma. MoEST